

# Somo la 3: Kazi ya Wokovu na Kuinuliwa

Unaweza kufundisha somo hili kwa ukamilifu au kuligawa katika sehemu fupi. Badilisha somo kwa hali ya eneo lako na mahitaji, umri, na uelewa wa urais wako wa akidi au wa darasa.

## KAZI YA URAIS WA AKIDI AU WA DARASA

Waalike washiriki wa urais kusoma pamoja *General Handbook: Serving in The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints*, 1.2 (ChurchofJesusChrist.org), na waalike watafute kazi ambayo Bwana amewaita waitimize. Kwa nini hii kazi ni muhimu? Ni nini tayari tunafanya ili kutimiza madhumuni haya? Ni malengo gani tunaweza kuweka au kurekebisha ili kufanikisha vyema madhumuni haya?

## KUSHIRIKISHA WASHIRIKI WA AKIDI AU DARASA KATIKA KAZI

Waombe washiriki wa urais wapitie kile walichojadili na kupanga kama urais. (Unaweza kutaka kuwaomba wapitie [Ajenda ya mkutano wa urais](#), pamoja na mipango yao ya huduma na shughuli.) Halafu uliza maswali yafuatayo:

- Ni kwa jinsi gani tayari tumefokasi kwenye kazi ya wokovu na kuinuliwa?
- Wapi tunaweza kuboresha?

Alika urais kujadili jinsi wanavyoweza kuwasaidia washiriki wao wa akidi au darasa kushiriki kikamilifu katika kazi ya wokovu na kuinuliwa. Maswali kama haya yafuatayo yanaweza kujadiliwa na urais au akidi au darasa:

- Je! Tunawezaje kusaidiana kuishi vizuri injili ya Yesu Kristo?
- Tunaweza kufanya nini kuwajali wale walio katika uhitaji?
- Je! Tunawezaje kuwasaidia wote kuhisi wamealikwa na kukaribishwa kujiunga nasi?
- Je! Tunawezaje kuhimiza ushiriki katika historia ya familia na kazi ya hekaluni?

Ona maswali mengine yanayowezekana katika sehemu ya “Shaurianeni kwa Pamoja” katika kila somo katika [Njoo, Unifuata—Kwa ajili ya Akidi za Ukuhani wa Haruni na Madarasa ya Wasichana](#).

## NYENZO SAIDIZI

- *General Handbook*, sura ya 1
- “Youth Responsibility in the Work of Salvation” video
- Carol F. McConkie, “Hapa Kutumikia Kusudi la Haki,” *Ensign* au *Liahona*, Nov. 2015, 12–14
- Waefeso 4:11–13; Moroni 10:32; Musa 1:39